

CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA KIBABII

**(CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA CHUO KIKUU CHA SAYANSI NA
TEKNOLOJIA CHA MASINDE MULIRO)**

KIS 200: NADHARIA NA UHAKIKI WA FASIHI

2013/2014

MAIN EXAM

MAAGIZO: JIBU MASWALI MANNE; SWALI LA KWANZA NI LA LAZIMA

1. (a) Eleza maana ya dhana zifuatazo huku ukitoa mifano.

(i) Nadharia. (alama 1)

Miongozo inayomsaidia msomaji wa kazi ya fasihi kuifafanua kazi ile kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa/ vinavyozalika kutokana na uchunguzi wa aina mbalimbali za fasihi/ jumla ya maelekezo yanayomsaidia msomaji au msomaji au mhakiki kuifahamu kazi ya fasihi kwa kufuata utaratibu maalum.

(kadiria majibu ya wanafunzi)

(ii) Uhakiki wa fasihi. (alama 1)

(Maelezo au maandishi yanayochambua maandishi/ masimulizi ya kifasihi kwa kufafanua mambo mbalimbali yaliyomo).

(b) Eleza aina saba za uhakiki . (alama 7)

Sadfa, marejeleo au bibliografia, uhariri, mapitio, ufundishaji, propaganda, upigaji marufuku, wa kitaaluma.

(Kutaja al. nusu kueleza al.nusu)

(c) (i) Eleza maana ya tanzia (alama 1)

(ii) Fafanua sifa za tanzia kwa mujibu wa Aristotle kwa kurejelea tamthilia ya *Mfalme*

Edipode. (alama 10)

Tanzia ni maigizo ya matukio yanayowasilishwa kwa lugha inayonawiri, yazindua hofu na huruma ili hatimaye maigizo hayo yaripue hisia za ndani kutoka katika nafsi ya hadhira.

Tanzia ina sehemu tatu; mwanzo, katikati na mwisho.

Tanzia huyakumba maisha ya nhusika mkuu

Jitihada haiondoi kudura

Vinyume vya mambo na kejeli huyakumba maisha ya mhusika mkuu; mhusika hujikuta katika hali zilizo kinyume na matarajio yake.

Mhusika tanzia ana fahari inayomsukuma hadi mwisho wa maisha yake-kiburi;

Wakati mwingine fahari hiyo huwa ni kiburi ambacho humsukuma mhusika kuishia katika hali ya kuhuzunisha. Ikumbukwe kuwa wakati mwingine si kiburi, yaweza kuwa nia njema kwa mfano, Edipode alinuia mema katika kuyatatua matatizo yanayokumba mji waThebe

Maadili hukusanywa na kutolewa na wazee kuhusiana na tajriba alizozipitia mhusika.

Mf. heshima kwa kila mtu. Huwezi kupigana na majaliwa

(mhimili al. 5 kutumikiza al. 5 jumla al. 10)

(d) Fafanua kwa kina sura mbalimbali za nadharia. (alama 5)

Mwongozo

Sheria za kutunga na kuhakiki kazi za fasihi

Mkakati wa kusoma

ujarabati katika kusoma kazi za sanaa

usomaji wa kimfumo

usomaji unaolenga kuwawezesha wanajamii kuwamiliki wengine

(Kutaja alama nusu kueleza al.nusu jumla hoja 5)

2. (a) Fafanua kwa tafsili vigezo vinavyotumika kuainisha nadharia bora. (alama 5)

Inafaa kutokana na majaribio mengi na uchunguzi mwingi,

Umfumo

Kuelezwa kwa ufasaha

Manufaa kwa muundaji na watumiaji

Kubadilika kwa kuitikia mabadiliko ya kijamii

(Kutaja alama nusu kueleza al.nusu jumla hoja 5)

(b) Kwa kutoa mifano, eleza tofauti kati ya nadharia asilia, nadharia nyambuaji na nadharia changamano. (alama 6)

Asilia – isiyotokana na nadharia nyingine, inajitosheleza.

Mfano uhalisia, urasimi, ulimbwende

Nyambuaji- inatokana na nadharia iliyokuwepo hapo awali / kimelea cha nadharia iliyotangulia. Mfano-urasimi mpya, ufeministi wa kiafrika.

Changamano- inatokana na nadharia mbili au zaidi. Mfano uhalisia wa kijamaa, ufeministi wa kidhanaishi.

(al 1 maelezo . mfano al 1 julma al. 2 kwa kila nadharia).

(c) Eleza umuhimu wa uhakiki kwa wasomaji wa kazi za fasihi. (alama 4)

Kuifanya kazi inayosomwa/ kusikilizwa kufahamika zaidi.

Kumzindua msomaji kupata mshawasha wa kuisoma kazi upya

Mwandishi anaweza kutilia maanani mambo ambayo pengine hangetilia maanani.

Mwandishi husaidiwa kwa kazi zinazofuata zile zilizohakikiwa. Mfano kurekebisha.

Kutoa tathmini iwapo kazi imefanikiwa.

(Kutaja alama nusu kueleza al.nusu jumla hoja 4)

3. (a) Eleza sifa za kijumla za urasimi. (alama 6)

Kazi za kirasimi huwasilishwa katika lugha inayoeleweka kwa urahisi;

uhalisia hutumiwa mtindo wa kinjozi hautumiwi

Haichoshi kusomwa

Maudhui na mtindo katika kazi hizi ni mambo yaliyifinyangwa kwa kutumia mbinu

kamilifu na teule.

Mwanasanaa anayetunga kazi ya kirasimi humezwa na mkondo wa fikra ulomzalisha.

(kila hoja al. 1 jumla al.6)

(b) Fafanua ujuzi wa wataalamu wafuatao kuhusu fasihi:- (alama 9)

(i) Plato

Chanzo cha fasihi ni jadh

Fasihi ni uigaji wa mazingira na hali nyingine anamopatikana binadamu

Fasihi inapaswa kuhakikiwa

Lengo la fasihi ni kuadilisha. Isipofanya hivyo ipigwe marufuku

(ii)Aristotle

Fasihi si uigo wa kikasuku. Ni ubunifu unaomwezesha binadamu kumkaribia Mungu.

Ploti/ msuko ni muhimu katika ubunifu wa sanaa; tanzia na uteni
Fasihi itaeleweka vizuri iwapo itagawanya katika tazu tofauti tofauti.

(iii) Horace

Fasihi lazima ilenge kuadili na kuisimua

Tamthilia lazima iwe na maonyeshi matano

Utungaji mzuri unatokana na uigaji wa kazi za watunzi mashuhuri walioishi zamani za kale.

(kila mtaalamu al. 3 jumla al.9)

4. Kwa kutumia *Utenzi wa Mwana Kupona*, eleza sifa za fasihi ya Kiswahili kwa kujikita katika misingi ya kirasimi. (alama 15)

Ndio wakati misingi ya ushairi wa Kiswahili iliwekwa

Mashairi yalipokezwa kwa midomo

Uhakiki ni kwa njia ya masimulizi

Utungaji ulitokana na mazingira

Lugha teule ilitumiwa katika ushairi

Lugha rahisi

Arudhi

Masimulizi marefu kama utenzi yana mwanzo kati na mwisho

(Utangulizi: Maana ya urasimi al. 1 Kuorodhesha mihimili al 7 utumikizi 8).

5. Chagua mojawapo wa nadharia zifuatazo kisha uonyesha jinsi inavyojitokeza katika kazi zozote za sanaa ulizosoma. (alama15)

(i) Ufeministi

Inatumia fasihi kama jukwaa hali aliyomo mwanamke

Kusawazisha hali ya mwanadamu kiuan na utamaduni

Kuhamasisha utungaji wa kazi za sanaa zenye wahusika wa kike wanaoweza kuigwa

Kuendeleza hisia za umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa

Kuzindua mwamko kwa upande wa wanawake jinsi wanavyojiona na wuhusika wengine

Kuvumbua na kuweka wazi kazi za fasihi zilizotungwa na wanawake zilizopuuzwa kwa sababu ya utamaduni unaompendelea mwanamume.

(ii) Usemezano

Fasihi ni uwanja wenye mwingiliano wa matini.

Sauti mbalimbali zinaingiliana na kupiga mwanangwi katika kazi nyinginezo zilizotangilia, zilizopo au zizkazokuja baadaye.

Hakuna matini asilia.

(iii) Umaksi

Maendeleo yaliyohusu jamii thabiti hutokana na vizazi alivyopitia binadamu

Tabaka la jamii hutoweka na linguine kutokea kwa sababu ya mgongano kati ya tabaka tawala na linalotawaliwa.

Mapinduzi hutokea kwa sababu ya mifumo ya kuzalisha mali inayohimili unyonyaji.

Mapinduzi yanalenga kuleta usawa.

Vidato vinavyopitiwa na jamii kabla ya kufikia ukamilifu wa kinjozi

Ujima, utumwa, umwinyi, ubepari, ujamaa, ukomunisti

(Kuorodhesha mihimili al 5 kutumikiza 10).

6. Fafanua mihimili ya nadharia ya Uhalisia wa kijamii huku ukirejelea tamthiia ya *Kilio cha Haki*, (alama 15)

Wahusika wa kimaendeleo

Husawiri matukio kihistoria, wahusika hutekeleza matukio yao kitabaka

Huzingatia maslahi ya makabwela

Binadamu huonyeshwa kiuyakinifu

Huonyesha matumaini juu ya kizazi cha binadamu

Lugha inayotumiwa inaendeleza malengo na mapendekezo ya walio wengi katika jamii

(Kuorodhesha mihimili al 5 utumikizi 10).

7. Kwa kujikita katika riwaya, ya *Utengano* (S. A. Mohamed), jadili baadhi ya matatizo yanayowakumba wanawake. (alama 10)

(Kutaja matatizo al. 1 kueleza al. 1 jumla al.10)

(b) Juhudi gani zinafanywa kutatua matatizo hayo. (alama 5)

(Suluhu kwa kila hoja al.5)

Kadiria majibu ya wanafunzi

CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA KIBABII
(CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA CHUO KIKUU CHA SAYANSI NA
TEKNOLOJIA CHA MASINDE MULIRO)

KIS 200: NADHARIA NA UHAKIKI WA FASIHI

2013/2014

SPECIAL/SUPPLIMENTARY

MAAGIZO: JIBU MASWALI MANNE; SWALI LA KWANZA NI LA LAZIMA

1. (a) Eleza maana ya dhana zifuatazo huku ukitoa mifano.

(i) Nadharia. (alama 2)

Miongozo inayomsaidia msomaji wa kazi ya fasihi kuifafanua kazi ile kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa/ vinavyozalika kutokana na uchunguzi wa aina mbalimbali za fasihi/ jumla ya maelekezo yanayomsaidia msomaji au msomaji au mhakiki kuifahamu kazi ya fasihi kwa kufuata utaratibu maalum.

(kadiria majibu ya wanafunzi)

(ii) Uhakiki wa fasihi. (alama 2)

Maelezo au maandishi yanayochambua maandishi/ masimulizi ya kifasihi kwa kufafanua mambo mbalimbali yaliyomo.

(kadiria majibu ya wanafunzi)

(b) Eleza maana ya tanzia kisha ufafanue sifa za tanzia kwa mujibu wa Aristotle kwa kurejelea tamthilia ya *Mfalme Edipode*. (alama 15)

(Kueleza maana kama sehemu ya utangulizi . Mwalimu akadirie)

Tanzia ni maigizo ya matukio yanayowasilishwa kwa lugha inayonawiri, yazindua hofu na huruma ili hatimaye maigizo hayo yaripue hisia za ndani kutoka katika nafsi ya hadhira.

Tanzia ina sehemu tatu; mwanzo, katikati na mwisho.

Tanzia huyakumba maisha ya nhusika mkuu

Jitihada haiondoi kudura

Vinyume vya mambo na kejeli huyakumba maisha ya mhusika mkuu; mhusika hujikuta katika hali zilizo kinyume na matarajio yake.

Mhusika tanzia ana fahari inayomsukuma hadi mwisho wa maisha yake-kiburi;

Wakati mwingine fahari hiyo huwa ni kiburi ambacho humsukuma mhusika kuishia katika hali ya kuhuzunisha. Ikumbukwe kuwa wakati mwingine si kiburi, yaweza kuwa nia njema kwa mfano, Edipode alinuia mema katika kuyatatua matatizo yanayokumba mji waThebe

Maadili hukusanywa na kutolewa na wazee kuhusiana na tajriba alizozipitia mhusika.

Mf. heshima kwa kila mtu. Huwezi kupigana na majaliwa

(Kutaja mihimili 5 al.5 kutumikiza alama 10)

(c) Eleza aina sita za uhakiki . (alama 6)

Sadfa, marejeleo au bibliografia, uhariri, mapitio, ufundishaji, propaganda, upigaji marufuku, wa kitaaluma.

(Kutaja al. nusu kuuleza al.nusu. hoja 6)

2. (a)Fafanua kwa kina sura mbalimbali za nadharia. (alama 10)

Mwongozo

Sheria za kutunga na kuhakiki kazi za fasihi

Mkakati wa kusoma

ujarabati katika kusoma kazi za sanaa

usomaji wa kimfumo

usomaji unaolenga kuwawezesha wanajamii kuwamiliki wengine

(Kutaja al.1 kueleza al.1 jumla al.10)

(b) Eleza umuhimu wa uhakiki kwa wasomaji wa kazi za fasihi. (alama 5)

Kuifanya kazi inayosomwa/ kusikilizwa kufahamika zaidi.

Kumzindua msomaji kupata mshawasha wa kuisoma kazi upya

Mwandishi anweza kutilia maanani mambo ambayo pengine hangetilia maanani.

Mwandishi husaidiwa kwa kazi zinazofuata zile zilizohakikiwa. Mfano kurekebisha.

Kutoa tathmini iwapo kazi imefanikiwa.

(Kutaja al. nusu kuuleza al.nusu. hoja 5)

3. Fafanua nadharia ya udhanaishi kwa kurejelea kazi yoyote ya Euphrase Kezilahabi.
(alama 15)

Maisha ni nini?

Uhusiano kati ya binadamu na Mungu kutokana na ugumu wake na kuvunjika kwa maadili ya jamii

Mungu amekufa - inamchora binadamu katika upweke wake

Binadamu ndiye chanzo cha ulimwengi na kama hangekuwepo ulimwengu haungokuwepo- si Mungu

Mtu huzaliwa/ kujipata katika ombwe la aina Fulani. Yuko huru kuishi tu katika ombwe hilo kuishi huku akikabiliana na ulimwengu unaomzunguka

Hana uwezo juu ya masuala kama maumivu basi anakata tamaa. Hata hivyo kabla ya kukumbwa na mauti atafanya matendo yanayotoa maana ya maisha yake

Maudhui ni kama kifo, uhuru wa mtu binafsi, wajibu wa binadamu duniani, ubinafsi kukata tamaa na udhaifu wa kibinadamu

Maisha ni usumbufu. Kwanini uzaliwe, eseke kisha ufe? Mtu hufa pale anapozaliwa.

(Mihimili 5 al.5 kutumikiza al.10)

4. (a) Eleza sifa za kijumla za urasimi. (alama 6)

Kazi za kirasimi huwasilishwa katika lugha inayoeleweka kwa urahisi

Uhalisia hutumiwa mtindo wa kinjozi hautumiwi

Haichoshi kusomwa

Maudhui na mtindo katika kazi hizi ni mambo yaliyifinyangwa kwa kutumia mbinu kamilifu na teule.

Mwanasanaa anayetunga kazi ya kirasimi humezwa na mkondo wa fikra ulomzalisha

(Hoja 6 al. 6)

(b) Jadili maoni ya Plato kuhusu fasihi. (alama 9)

Chanzo cha fasihi ni jadhba

Fasihi ni uigaji wa mazingira na hali nyingine anamopatikana binadamu

Fasihi inapaswa kuhakikiwa

Lengo la fasihi ni kuadilisha. Isipofanya hivyo ipigwe marufuku

(Hoja 3 al.3 ufafanuzi al 6 jumla al. 9. Kadiria majibu)

5. (a) Fafanua ujuzi wa Horace kuhusu fasihi kwa kurejelea kazi yoyote ya kisanaa uliyosoma. (alama 4)

Fasihi lazima ilenge kuadili na kuisisimua

Tamthilia lazima iwe na maonyeshi matano

Utungaji mzuri unatokana na uigaji wa kazi za watunzi mashuhuri walioishi zamani za kale.

(Hoja 1 al. 1 maelezo al 1 jumla al.4)

(b) Fafanua kwa tafsili vigezo vinavyotumika kuainisha nadharia bora. (alama 5)

Inafaa kutokana na majaribio mengi na uchunguzi mwingi,

Umfumo

Kuelezwa kwa ufasaha

Manufaa kwa muundaji na watumiaji

Kubadilika kwa kuitikia mabadiliko ya kijamii

(Kila hoja al. 1 jumla al.5)

(c) Kwa kutoa mifano, eleza aina tatu za nadharia. (alama 6)

Asilia – isiyotokana na nadharia nyingine, inajitosheleza.

Mfano uhalisia, urasimi, ulimbwende

Nyambuaji- inatokana na nadharia iliyokuwepo hapo awali / kimelea cha nadharia iliyotangulia. Mfano-urasimi mpya, ufeministi wa kiafrika.

Changamano- inatokana na nadharia mbili au zaidi. Mfano uhalisia wa kijamaa, ufeministi wa kidhanaishi

(Maelelezo al. 1 mf. Al.1)

6. Kwa kutumia *Utenzi wa Mwana Kupona*, eleza sifa za fasihi ya Kiswahili kwa kujikita katika misingi ya kirasimi. (alama 15)

Ndio wakati misingi ya ushairi wa Kiswahili iliwekwa

Mashairi yalipokezwa kwa midomo

Uhakiki ni kwa njia ya masimulizi

Utungaji ulitokana na mazingira

Lugha teule ilitumiwa katika ushairi

Lugha rahisi

Arudhi

Masimulizi marefu kama utenzi yana mwanzo kati na mwisho
Kuorodhesha mihimili al 7 utumikizi 8.

7. Chagua mojawapo wa nadharia zifuatazo kisha uonyesha jinsi inavyojitokeza katika kazi zozote za sanaa ulizosoma.(alama 15)

(i) Ufeministi

Inatumia fasihi kama jukwaa hali aliyomo mwanamke

Kusawazisha hali ya mwanadamu kiuan na utamaduni

Kuhamasisha utungaji wa kazi za sanaa zenye wahusika wa kike wanaoweza kuigwa

Kuendeleza hisia za umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa

Kuzindua mwamko kwa upande wa wanawake jinsi wanavyojiona na wuhusika wengine

Kuvumbua na kuweka wazi kazi za fasihi zilizotungwa na wanawake zilizopuuzwa kwa sababu ya utamaduni unaompendelea mwanamume.

(ii) Usemezano

Fasihi ni uwanja wenye mwingiliano wa matini.

Sauti mbalimbali zinaingiliana na kupiga mwangwi katika kazi nyinginezo zilizotangilia, zilizopo au zitzkazokuja baadaye.

Hakuna matini asilia

(iii)Umaksi

Maendeleo yaliyohusu jamii thabiti hutokana na vizazi alivyopitia binadamu

Tabaka la jamii hutoweka na lingine kutokea kwa sababu ya mgongano kati ya tabaka tawala na linalotawaliwa.

Mapinduzi hutokea kwa sababu ya mifumo ya kuzalisha mali inayohimili unyonyaji.

Mapinduzi yanalenga kuleta usawa.

Vidato vinavyopitiwa na jamii kabla ya kufikia ukamilifu wa kinjozi

Ujima, utumwa, umwinyi, ubepari, ujamaa, ukomunisti.

(iv)Uhalisia wa kijamii

Wahusika wa kimaendeleo

Husawiri matukio kihistoria , wahusika hutekeleza matukio yao kitabaka

Huzingatia maslahi ya makabwela

Binadamu huonyeshwa kiuyakinifu

Huonyesha matumaini juu ya kizazi cha binadamu

Lugha inayotumiwa inaendeleza malengo na mapendekezo ya walio wengi katika jami

Kuorodhesha mihimili al 5 kutumikiza 10.